NA TANGU WAKATI HUO

Hakika ni vema kurudi na kumsikia huyu ndugu, mchungaji, akitoa ushuhuda wa neema ya Mungu, pamoja na msichana wake mdogo. Huyo ni kama tu Bwana Yesu, kufanya mambo namna hiyo. Hakika ndivyo.

2 Sasa, tuna furaha sana, usiku wa leo kuwa pamoja nasi, mmoja wa wageni wetu hapa kwenye, kama tunavyoiita, ibada ya maombi kwenye usiku wa Mwaka Mpya, rafiki yangu mwema, Ndugu Ernie Fandler, mmoja wa waongofu wa Bwana Yesu Kristo, kumbukumbu ya neema. Asili ya makazi yake ni Switzerland, ndiko alikotoka. Nami naamini, ndugu pamoja naye kule, ambao wanaishi Shawano sasa, asili yake ni Mjerumani, Ndugu Waters. Tuna furaha kuwa pamoja nao usiku wa leo.

3 Halafu tunaye, pia, usiku wa leo, ndu—ndugu wa thamani wa imani, Afrika Kusini, Ndugu David duPlessis. Tuna furaha kuwa naye, pia. Na sisi, mimi na David, tuna—tunatazamia, tunaomba, katika Bwana, kutupatia kazi kuu pamoja, mwaka huu ujao, kuingia Afrika na sehemu mbalimbali za ulimwengu. Ndugu David yuko hapa sasa kulizungumzia, na kuomba kwa ajili yake, kati ya sasa na Jumatatu, kuamua ni wakati gani na ni kwenda wapi, ka—katika Afrika, na sehemu mbalimbali za ulimwengu. Vile, Ndugu David amekuwa na ofisi maarufu sana pamoja na Mkutano wa Kipentekoste Ulimwenguni, na pia anajulikana sana na viongozi wakuu wa dini kote ulimwenguni. Na amekuwa na ushawishi mwingi katika kuwasihi na kuwafanya, kufikia umbali tulipo sasa, kusaidia kuuleta Mwili wa Yesu Kristo pamoja, wa madhehebu yote ya imani. Bila kujali kile (wao) kanisa lilicho nacho, ama (wao) wamepigwa chapa gani. Ni lile, Kanisa, Ambalo Kristo alifia.

4 Nami mara nyingi nimeliwazia jambo hilo. Nilikuwa nikisaidia kuwakusanya ng'ombe, mara nyingi, huko Magharibi. Tungepanda juu, Ndugu David, na kuketi huko nje ambako waliwapitisha ng'ombe kwenye uzio unaohama, kuwapandisha milimani, kuwalisha kwenye. . . kuwaacha wale majani kwenye malisho, ninii. . . ya mwituni. Wakati, makonde ya majani yalikuwa yakikua huko chini, makonde mwitu. Ndipo wakafyeka hayo makonde, na kuwalisha ng'ombe kote—kote katika majira ya baridi kali, wakati kukiweko na dhoruba kali ya theluji, huko juu milimani.

5 Nami nilikuwa nikiketi kule juu ya matandiko na kumwangalia mlinzi akiwapitisha hao ng'ombe; na kila ranchi, huko chini, ambayo ingeweza kuchangia tani moja ya nyasi kavu. Kama wangeweza kuchangia tani hamsini ya nyasi kavu, hiyo

ilimaanisha wangeweza kuwaweka ng'ombe hamsini. Kama wangeweza kuchangia tani elfu moja ya nyasi kavu, ng'ombe elfu moja wangeweza kupitishwa. Kila mtu, akiwa amebeba chapa kwenye ng'ombe wake. Waliangalia hizo chapa, hakika, ranchi mbalimbali, wasije wakachanganyikana. Ndipo wakati ninii . . .

6 Huyo mlinzi, yeye hakuvutiwa sana na aina za chapa zilizokuwa zikipita, kwa sababu kulikuwako na kila namna za chapa. Ila kulikuwako na kitu kimoja ambacho kweli ilimbidi kuchunguza, hicho kilikuwa ni alama ya damu. Ilibidi wawe ni Hereford waliosajiliwa, la sivyo wasingeweza kupitia langoni. Waliwarudisha. Mnaona?

7 Pia nadhani ndivyo itakavyokuwa kwenye ile Hukumu. Haitakuwa ni chapa ya aina gani tunayovaa, bali kama alama ya Damu ipo. Hicho ndicho kitu kita—kitakachojalisha, alama ya Damu.

Nami nina furaha sana kuwa na Ndugu David pamoja nasi.

8 Nami naona Ndugu Estle Beeler alikuwa hapa muda mfupi tu uliopita. Nilimwona akisimama kule nyuma, kutoka mahali fulani. Na wahudumu wengine ambao tunataka kusikia kutoka kwao, usiku wa leo. Na, halafu, basi nadhani Ndugu Ruddell na hao wengine watakuja, maana watakaa mpaka usiku wa manane.

9 Hata hivyo, Ndugu David hawezi kukaa mpaka usiku wa manane. Ni mtu anayehitajika sana, kila mahali. Na mara Ndugu Rodgers aliposikia ya kwamba alikuwa hapa, mbona, yeye ataagizia na kuwa naye kule saa nne. Kwa hiyo hiyo inamaanisha ataondoka hapa, muda mfupi sana, kwenda hadi huko Louisville ya kusini.

10 Nami nikawazia lingekuwa ni jambo jema, kama ingekuwa ni sawa na Ndugu David, ka—kama tungemfanya aje huku na kuzungumza yaliyo moyoni mwake, atuhubirie, afanye lolote Bwana analoweka. Sote tungetaka kumsikia Ndugu David duPlessis, kutoka Afrika Kusini.

11 Hebu niseme hili. Kwamba, nilipokuwa huko, huko Afrika, katika ule uamsho wangu mkuu Bwana aliotupa huko, kaka yake alikuwa ndiye mkalimani wangu, Ndugu Justus. Ninaamini jina lake ni Ndugu Justus. Nao ni familia nzuri sana ya watu, hawa ndugu wa duPlessis. Nafikiri kuna . . . Nadhani wote ni wahudumu, nijuavyo mimi, na labda baba, pia, ambaye alikuwa ni mhudumu. Nao wametoka kwenye familia nzuri ya watu. Naye Ndugu David ana jina kuu miongoni mwa makanisa yote na madhehebu kote ulimwenguni.

12 Nawe Ndugu David, ningetaka uje huku sasa na kutuzungumzia, ama lolote Mungu aliloweka moyoni mwako kusema. Panda huku moja kwa moja. Nami nina furaha sana kutambulishia kanisa langu, usiku wa leo. Huyu ni Ndugu

Orman Neville, mchungaji wetu. Na kwa kanisa, huyu ni mmoja wa marafiki zangu wa thamani, na—na askari wenzangu katika utumishi wa Mungu, Ndugu David duPlessis wa Afrika Kusini. Mungu akubariki, Ndugu David.

13 [Ndugu David duPlessis anazungumza. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ongea. Amina. Sote tulifanya hivyo. Ndugu David, fanya haraka urudi na uwe nasi tena. Hilo ni zuri sana. Hakika tumefurahi.

14 Ndugu David alisema mambo fulani hapo, laiti ningelikuwa na kalamu yangu, ningeliweza kuyaandika. Bali sikuzote nitakumbuka "wajukuu wa kiume; wajukuu."

15 Vema, hakika tunathamini kutembelewa na ndugu yetu. Naye ni . . . alikuwa . . . ana uhusiano na Kongamano la Ulimwengu la waaminio wa Kipentekoste, na ni mtu mashuhuri katika wadhifa wa kazi yake kote ulimwenguni. Nasi tumebahatika, usiku wa leo, kuwa na Ndugu David kuja kutuzungumzia kwenye usiku huu wa Mwaka Mpya. Nanyi mnaweza kuona yale watu mashuhuri wanayowazia juu ya Bwana wetu, juu ya mtumishi Wake mashuhuri.

16 Sasa ninaamini kwamba, kesho, ikiwa ni siku ya Mwaka Mpya, ni saa chache tu sasa. Nami sina budi kuondoka asubuhi na mapema, kwa hiyo niliwazia ningezungumza tu kidogo, kama ni sawa na Ndugu Neville. [Ndugu Neville anasema, "Naam. Amina."—Mh.] Ndugu Beeler, na wahudumu wengine hapa. Sitachukua wakati mwingi. Nami nafikiri, kama tungesema "Amina," na kwenda nyumbani, ungekuwa ni ujumbe mzuri sana. Nasi tunaweza kumshukuru Bwana kwa yale ambayo tunayo hapa, usiku wa leo.

17 Na sasa, lakini huu ukiwa ni usiku wa Mwaka Mpya, tunajifurahisha tu mmoja na mwenzake, kwa Ufalme wa Mungu, tukihubiri, mpaka ifikie Mwaka Mpya. Na sina budi . . . kuamka asubuhi, mapema sana, kabla ya mapambazuko. Wala mimi sio mchanga kama David. Labda mimi . . . Labda sijisikii mchanga kama anavyojisikia. Yeye ni . . . Bila shaka, David kidogo ni—kidogo ananizidi umri. Nadhani amenizidi umri kwa miaka saba ama minane, labda kumi. Lakini hakika yeye ni kimondo kwa ajili ya Mungu, akisafiri maili elfu hamsini mwaka huu, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Yuko njiani sasa kwenda kuhubiri kwa Ndugu Rodgers, na kesho awe na wengine, mahali pengine, na mahali pengine, na mahali pengine, kisha arudi hapa tena Jumatatu. Nami sina budi kukutana naye kufanya matayarisho ya ziara ya ulimwenguni kote inayokuja sasa.

18 Nasi tunapaswa kuwa Afrika, nilisikia alasiri hii, mnamo Machi, hii—hii Machi ijayo. Ninafaa kukutana na Clayton Sondmore, kutoka kwa Wafanyabiashara Wakristo wa Full Gospel, wiki hii, au wiki hii ijayo, sehemu yake ya kwanza, na kufanya maandalizi kwa ajili ya Jamaika, Haiti. Ninaenda

Kentucky juma lijalo, ama kushuka Georgia, kufanya hiyo mikutano kule. Nirudi mumu humu na kushuka kupitia Kentucky, usiku hapa, na usiku kule, kuyashika makanisa haya. Kisha nirudi moja kwa moja nyumbani kutoka huko, halafu niende hu—hu—huko Atlantic City, kwa kuwa unaanza kwenye tarehe 27, hadi 30, na kuondoka huko asubuhi ya tarehe 1, na kuanzia Ki—Kingston, Jamaika, kwenye uwa-. . . uwanja wa mashindano ya farasi, usiku huo, kwa mkutano wa siku kumi huko. Na tangu hapo na kuendelea, kisha kwenda Haiti, na popote pale. Hatujui twende wapi kutoka huko, kama vile tu Bwana atakavyotuongoza.

19 Sasa, haya yote yako kwenye maandalizi. Mnaona? Sijasema ndiyo. David yuko hapa, Clayt yuaja. Gordon, Ndugu Gordon Lindsay anakuja, kwa ajili ya Marekani Kusini. Na—nao hao wengine, Wafanyabiashara Wakristo kwa ajili ya Marekani inayozungumza Kilatini. Naye Ndugu David anaelekea Uswisi, Ujerumani, na kuendelea. Lakini hatujui bado. Nyinyi endeleeni kuomba. Sitaki kwenda popote mpaka Mungu anaposema niende, na kadri nijuavyo mimi. Kwa hiyo, kama nikijisikia kuongozwa kwenda, basi nikishuka kwenye ndege, mimi . . . Basi haidhuru upinzani ukoje, ninaweza kusema, “Nimekuja katika Jina la Bwana Yesu.”

20 Nilishukuru kwa ajili ya David, ule urafiki ambao tumekuwa nao pamoja, kwa sababu mtu huyo ni mtu muhimu sana, lakini yeye—yeye—yeye hakika anaamini huduma hii ya Bwana. Hakika anaiamini. Na—na majina yetu yamehusishwa pamoja ulimwenguni kote sasa, mimi na Ndugu David.

21 Nami nina furaha sana kuwa na uhusiano na mtu kama huyo. Bali, marafiki, ninathamini hilo. Lakini kitu muhimu kuliko vyote ambacho ninaweza kuwazia kuhusishwa nacho ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Yule aliye mkuu.

22 Sasa, Ndugu Neville na wengine wao watakuwa wakizungumza katika dakika chache, lakini ninataka kusoma kitu kidogo tu kutoka kwenye Maandiko sasa.

23 Na ni vizuri, nafikiri, kwenye usiku wa Mwaka Mpya, kuona wahubiri mbalimbali, na jinsi wanavyoliendea fungu la maneno, na kile wanachosema, na kadhalika. Na kila mtu akiwa na njia yake mwenyewe ya kuhubiri. Mnajua, Mungu hakutufanya sote sampuli moja. Alituumba tofauti. Alituumba tofauti katika kimo chetu. Aliumba dunia tofauti, na milima mikubwa, milima midogo, nyanda za majani, majangwa, maua makubwa meupe, maua ya samawati, na aina zote mbalimbali. Yeye hutuumba tu tofauti. Ni hayo tu. Yeye hufanya kichwa chekundu, na vichwa vyeusi, vichwa vya hudhurungi, kichwa cheupe; mnene, mwembamba, mrefu, loo, kadhalika. Mnaona? Yeye tu—Yeye hutufanya tu tofauti. Mungu ni Mungu wa vitu vya namna mbalimbali. Na kwa namna fulani napenda hilo. Nanyi je?

[Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Lakini kitu kile kile tu wakati wote? Jamani! Jamani! Napenda hili.

24 Kwa hivyo na tufungue sasa katika Maandiko yetu, kwenye Kitabu cha Mathayo Mtakatifu, Injili ya Mathayo Mtakatifu, kuanzia kwenye . . . Na kifungu cha 4, ninataka kusoma kwa ajili ya . . . kutusomea fungu la maneno, Bwana akitusaidia. Mathayo Mtakatifu, sura ya 4.

Ninaamini, kabla hatujasoma, hebu tuombe.

25 Baba wa Mbinguni mwenye neema, ni kwa mioyo yenye shukrani tena ambapo tunaukaribia mwaka huu mpya. Na tunakukaribia Wewe na tunakuletea kila masumbuko yetu ya wakati uliopita, na kuomba kwamba utayaweka katika bahari ya usahaulifu, wala usizikumbuke dhambi zetu dhidi yetu tena. Na jalia tusikague hali yetu ya kiroho pekee, lakini katika ninii yetu . . . jalia tuchunguze ushirika wetu pamoja na Wewe. Na utusamehe dhambi zetu zote. Nasi tunaomba kwamba Roho Wako atashughulika nasi usiku wa leo. Na kukiwako na kitu chochote kichafu kutuhusu, Bwana, kipeleke mbali kama mashariki ilivyo mbali na magharibi. Kitupe kwenye bahari ya usahaulifu, usikikumbuke dhidi yetu tena, ili tuweze kuingia katika mwaka huu mpya, safi, tumesafishwa kwa Damu ya Mwana-kondoo, na kuwa tayari.

26 Jalia mwaka huu wa 1960 uwe mwaka mkuu zaidi ambao tumewahi kukutumikia. Tujalie zaidi, kwa wingi sana. Mikutano hii yote inayoendelea, Bwana, ambayo tunaifikiria pamoja na Ndugu duPlessis, na kote ulimwenguni, kuingia Asia, na hadi huko Ulaya, na kote—kote kote. Bwana, jalia iwe mapenzi Yako na Nguvu Zako ambazo zitatuongoza kwenye vitu hivi. Na ikiwa wakati wowote tungetoka kwenye njia Yako ya Kiungu iliyoamriwa, jalia Roho Mtakatifu aweke kizuizi njiani na kutuzuia, Bwana, na kuturudisha mahali pafaapo. Lijalie.

27 Bariki kanisa hili dogo, Bwana. Karibu, karibu miaka thelathini, nadhani, limesimama hapa sasa, kama kumbukumbu ya neema ya Mungu, kwa watu wanyenyekevu. Tunaomba, Baba, kwamba utambariki Ndugu Neville, mchungaji. Bariki kanisa lote. Wabariki wadhamini, mashemasi, kiongozi wa nyimbo, mpiga piano, na walei wote, kila mmoja, waalimu wa shule ya Jumapili, kadhalika. Bwana, tuweze kukua mwaka huu katika neema ya Mungu. Na jalia ushirika wetu ukue kufikia idadi kubwa zaidi, na—na neema Yako zaidi, hata, kuliko jinsi hii imekuwa katika miaka iliyopita. Lijalie, Baba.

28 Sasa tusaidie tunapoliendea andiko hili tunalojiandaa kusoma, Neno Lako. Na ni Wewe tu, Bwana, unayeweza kutafsiri na tunaomba kwamba utatujalia, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

29 Natangaza hivi sasa lile nimechagua kama somo kwa dakika zingine chache zijazo. Linapatikana katika Maandiko

hapa, nami nitayasoma. Ni kuliita, nataka kuliita hivi, "tangu wakati huo."

30 Sikufikiria, nilisema hivi majuzi usiku, sikudhani ningeweza kushuka huku, kwa sababu koo langu lilikuwa likipwelewa na sauti. Ndipo mke wangu aliniambia jana, au siku moja kabla, alisema, "Basi nadhani hutashuka kwenda kanisani."

31 Nikasema, "Mpendwa, sidhani. Koo langu linauma sana na ni bichi."

32 Halafu, jana usiku tu, wakati nilipoketi chini na kuchukua Maandiko, nililipata Hili.

33 Ndugu Sothmann akapitia hapo. Akasema, "Je, utaenda kanisani kesho usiku?"

Nikasema, "Naam. Nitakuwa huko."

34 Naye Meda akanitazama, na akasema, "Sikuelewi."

Nikasema, "Sikutarajii uelewe, unaona," nikasema, "wala mtu mwingine."

35 Hakuna mtu anayeongozwa na Roho wa Mungu anayeweza kueleweka.

36 Bwana wetu, hawangeweza kumwelewa. Alionekana kana kwamba aliongea kwa njia moja, dakika moja; na njia nyingine, dakika nyingine. Na mahali pengine alikuwa akizungumza juu ya kitu kingine. Wakati mwingine ilikuwa ni Yesu akiongea, wakati mwingine ilikuwa ni Mungu akiongea. Mnaona? Hata wanafunzi walisema hapo, mwishowe, wakasema, "Tazama, sasa wasema waziwazi. Sasa tunaelewa." Mnaona?

37 Naye Yesu akasema, "Je, mnae-. . .Na sasa mnasadiki?" Mnaona, baada ya hapo.

38 Kamwe huwezi kuifanya, kwa sababu unaongozwa na Roho. Na unaanza kufanya jambo, unagundua kwamba, unaona, uko. . .Mungu anataka kukutumia mahali fulani. Unapaswa kusimama *hapa* na kwenda *hapa,* ukiongozwa tu na Roho. Wao ni watu wasio wa kawaida, watu wa kipekee ambao wana maisha ambayo unataka kuyaweka wakfu kwa Mungu.

39 Na kisha sikuzote mimi husema hivi, "Nitafanya hivi Bwana akipenda." Unaona? Kama nikimtolea ahadi mtu yeyote, "Nitafanya hivyo Bwana akipenda." Unaona? Na kwa hivyo, basi, ikiwa sio mapenzi ya Bwana, nitakuwa. . .Nitazungumza juu ya Ujumbe huu Bwana akipenda. Angeweza kunipa wito, moja kwa moja katika Ujumbe huu, nitoke niende California. Ningeweka kando kila kitu na kwenda California, upesi niwezavyo kwenda.

40 Nami nataka kuishi namna hiyo. Sitaki kitu chochote kinifunge. Sitaki kitu chochote kikubwa ama chochote kile, ambapo kina thamani ya mamilioni ya dola, na inakubidi kupata pesa nyingi, kila siku, kunifunga. Nataka kuwa, ambapo, Mungu

anaposema, "Nataka ushuke hapa kwa watu hawa. Ni watano tu. Lakini shuka uende kule chini, ukae huko mpaka nikwambie uondoke." Nataka kwenda huko. Sina wajibu wowote, ninii tu . . . na ikiwa anataka niende nchi za ng'ambo.

41 Sasa hii hapa, ndiyo kwanza itajwe, kwenda Ujerumani, au kwenda—kwenda Afrika. Basi mwanamke mmoja milionea, wakati tu ambao Roho aliliweka juu yangu kwenda Afrika, alisema, "Nitaifadhili hiyo safari na kulipia kila sehemu yake." Mnaona? Hamna lingine. Kwa nini nihofu juu ya pesa na kadhalika, wakati Baba yangu anazimiliki zote? Mnaona? Anaweza tu kuzungumza na mtu huyu tajiri, ama mtu yule tajiri, ama watu hawa, ama watu wale, wala sina haja ya kuhofu juu yake. Mnaona? Mungu hulishughulikia lote tu.

42 Ndugu Roy, hiyo ndiyo njia ya kuishi. Kumwacha tu alishughulikie. Ni vema sana.

43 Sasa hebu tuyafungue Maandiko yetu, kwenye mlango wa 4. Na hebu tuanze ku—kusoma, kwenye kifungu cha 12 cha mlango wa 4 wa Injili ya Mathayo Mtakatifu.

> *Sasa wakati Yesu* alikuwa . . . Basi *Yesu aliposikia ya kwamba Yohana ametiwa gerezani, alikwenda zake* mpaka *Galilaya;*
>
> . . . *akatoka Nazareti, akaja akakaa Kapernaumu, mji ulioko pwani, mipakani mwa Zabuloni* huko *Naftali:*
>
> *Ili litimie neno lililonenwa na nabii* Isaya, *akisema,*
>
> *Nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali, Njia ya bahari, ng'ambo ya Yordani, Galilaya ya Mataifa;*
>
> *Watu* wale *waliokaa katika giza wameona mwanga mkuu; nao waliokaa katika* maeneo ya *uvuli wa mauti, mwanga umewazukia.*
>
> *Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, Tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.*

44 Ninataka kuzungumza juu ya somo: *Na Tangu Wakati Huo*. Mnajua, kama mwanadamu, sisi sote tunayawazia mambo kutoka wakati fulani. Kitu hiki na kile kilitukia, na tangu wakati huo. Na sasa, mara nyingi, unakutana na mwanamume mzee ama mwanamke mkongwe, nao wanapenda kurejea kwenye wakati ambapo jambo fulani lilitukia, ambapo wanaweza kuukumbuka vizuri na kusema, "Ilikuwa ni wakati huo."

45 Sasa, nadhani kuna karibu sisi sote hapa, usiku wa leo, tunaweza kukumbuka, kumbukumbu ya mambo fulani yaliyotukia kwenye wakati fulani. Tangu wakati huo, kitu fulani kilibadilika. Kitu *fulani-fulani*, kilitukia wakati huo. Na tangu wakati huo na kuendelea, ilikuwa ni tofauti. Na ni jambo jema kwamba tunaweza. Na baadhi ya kumbukumbu hizo za mambo

tunayoyakumbuka, ni mambo muhimu yaliyobadilika. Na kuna mambo ambayo hayana faida sana kuyakumbuka.

46 Kwa mfano, kama mwanamke mwenye sifa mbaya, ambaye alisema, "Kulikuwako na wakati nilipokuwa msichana mzuri, mwenye haki, mwadilifu. Basi usiku mmoja, ama mahali fulani, jambo fulani lilitukia." Na tangu wakati huo, amekuwa kwenye njia mbaya. Maisha yake yamechafuliwa na dhambi, na weusi na giza, na hukumu tu ndiyo inayomngojea. Lakini anaweza kukumbuka, tangu wakati huo fulani, lilitukia wakati alipoichukua njia mbaya.

47 M—mlevi, usiku wa leo, mitaani, anayejaribu kuyasahau majonzi yake kwa kuyanywea pombe. Unaweza ukamwinua juu. Kama vile nilivyokuwa kwenye kituo cha walevi hapa, siku moja, huko New York, kile kituo kikuu cha walevi. Nilikuwa nikiongozana na mhudumu fulani. Basi hapo alilala mtu, loo, watu wengi tu, wasio na madhara, wasiojiweza, wamelala pale huku upande wa mbele wa nguo zao umelowa kabisa, na—na ndevu kote nyusoni mwao, na wakiwa tu katika hali mbaya sana. Nao kabisa walikuwa hawana madhara.

48 Ndipo mhudumu huyu akasema, "Hebu mwinue huyo juu, na umwulize tu."

49 Nikamwendea mtu huyu ambaye alikuwa amelala mguu mmoja umewekwa juu ya bamba la gari, nacho kichwa chake kimelala barabarani, na ambapo alikuwa hawezi kwe—kwe—kwenda nyakati zingine, msalani. Loo, alikuwa tu katika hali mbaya sana. Ndipo nikamshika, na kusema, "Unaweza kuzungumza?" Wala asingenijibu.

50 Ndipo huyu mhudumu akainama. Alijua zaidi jinsi ya kumshughulikia. Basi akamwuliza, "U nani wewe?"

51 Basi hatimaye akamwamsha vya kutosha, hata angeweza kusema, "Kama utaninunulia pombe!" Ndipo tukaja kugundua, angeweza kuelekeza kidole chake kwenye benki ambayo alikuwa rais wake.

52 "Vema," akasema, "sisi ni wahubiri. Unaweza kuniambia kilichotukia?"

"Kama utaniahidi pombe!"

53 Vema, tusingeweza kufanya hivyo. Nikasema, "Nisingeweza kuongeza huzuni kwenye huzuni zako. Nataka kukusaidia."

54 Hadithi yake yote. Yeye alirudi nyumbani, usiku mmoja, na kulikuwa na, kile alichokiita, barua ya "Mpendwa John" me—mezani. Basi, mke wake alikuwa amemwacha. Naye alikuwa . . . Alimpenda. Naye alikuwa amewachukua watoto wake. Naye alitalikiwa, naye alikuwa ametoroka na mwanamume mwingine. Ndipo akasema, "Sikujua la kufanya, kulipua ubongo wangu kwa risasi, ama nifanyeje. Kwa hiyo ni—nikatelemka

kwenye baa." Na tangu wakati huo, huyo hapo. Hiyo ni kote ulimwenguni.

55 Mwongo. Unaweza kumchukua mmoja, kama vile nilivyomwambia mtu fulani, siku moja, ambaye nilifikiri alikuwa anafanya mizaha. Ndipo nikaja kugundua, ya kwamba, yeye alisema uongo mwingi sana hata hatimaye akauamini, yeye mwenyewe. Ndipo nikasema, "Ni kitu gani kinachokufanya ufanye hivyo?" Ndipo nikaketi chini kuzungumza naye. Nikasema, "Nataka kukuuliza. Hadithi hizo ni za kishenzi sana kwa watu kuziamini."

56 Akasema, "Ya kwanza ninayoweza kukumbuka nikisimulia," akasema, "Nilikuwa mvulana mdogo aliyelelewa kweye nyumba nzuri." Kisha akasema, "Nilitoka nikaenda na kuvuta sigara za misogoro ya mahindi, kujifanya tu wa kisasa. Kisha nikala kahawa, ili kuiondolea mbali kwenye pumzi yangu." Naye akasema, "Nilifanya hivyo nyuma ya dohani la kale, nyuma ya nyumba." Kisha akasema, "Kamwe sitasahau, wakati mama aliponishika, na kuniambia, 'Mwanangu, hebu ninuse pumzi yako.' Nami nikaipulizia pumzi yangu usoni mwake, naye akasema, 'Umekula kahawa kuondolea mbali kitu kwenye pumzi yako. Kwani umekuwa ukifanya nini? Umekuwa ukivuta sigara?'"

57 Naye akasema, "Kitu fulani kikaniambia nimwambie ukweli." Akasema, "Lakini nikasema, 'La, mama. Ninakuapia. Sijawa nikivuta sigara.'" Akasema, "Na tangu wakati huo, hilo lililianzisha."

58 Sote tunaweza kupata kitu ambacho—ambacho kilianza kwenye wakati fulani. Na tangu wakati huo na kuendelea, mambo yalibadilika. Na kuna mambo mengine yenye faida ambayo tungeweza kuwazia. Watu wenye nia nzuri wamejaribu kuanzisha mambo upya, kufanya vitu wakati fulani.

59 Kwa mfano, wakati umeme ulipogunduliwa kwanza na Benjamin Franklin, nao walikuwa na uwezo kuushinda. Walianza kusema, "Tangu wakati huu na kuendelea, kamwe hakutakuwako na vita tena. Kwa sababu, kwamba, umeme huu ungeweza kuwekwa nyuani, ukiwa na volteji kubwa hivyo, hata hakuna mtu angaliweza kuuvuka." Walikusudia mema.

60 Na mara baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia, wakati—wakati Kaiser Wilhelm alipotia saini mkataba wa amani. Tuliambiwa hapa Marekani. Nilikuwa mvulana wa yapata umri wa miaka tisa. Lakini ninaweza kukukumbuka watu wote wakisema, "Kamwe hatutakuwa na vita tena. Tangu wakati huu na kuendelea, vimesuluhishwa, milele." Lakini tulikuwa na vita vingine.

61 Ndipo wakati U.N. kuu. Ama, ningesema, kabla ya hapo, waliunda lile lililoitwa Shirikisho la Taifa. Nao wakasema "Sasa hatutakuwa na vita tena, kwa sababu tuna Shirikisho la Mataifa

ambalo litaufanyia ulimwengu doria. Na endapo kuna maasi mahali fulani, watu hawa kutoka kila taifa wataenda kule na kuuchunga ulimwengu." Lakini ilishindwa. Waliendelea moja kwa moja wakiwa na vita. Nayo U.N. itakuwa ni kitu kile kile.

62 Tunaambiwa sasa kwa ubashiri ya kwamba kesho usiku ama Jumapili usiku . . . Mtu yule yule aliyebashiri Pearl Harbor, kufikia wakati ule ule hasa zi—zile ndege zingeirushia bomu, alisema, ya kwamba, "Jumapili usiku saa sita, kwamba asilimia sabini na tano ya Wamarekani watakuwa majivu, ya kwamba Urusi itaipiga Marekani bomu, Jumapili hii ijayo saa sita usiku." Mtu yule yule aliyebashiri Pearl Harbor. Hawalitangazi, maana watu wataingia wazimu. Siliamini. Mnaona? La. Kwa sababu, haiwezi kustahimili vita vya atomiki. Moja ya zao ilipita mapatano ya spidi ya sauti na ya ndege, *huku*, tutazitupa *huko*, nao ulimwengu utavunjika vipande vipande. Jambo fulani halina budi kutukia, bado, kabla ya Yesu kuja. Hiyo ni kweli.

63 Kwa mfano, vijana waliofunga ndoa. Kuna wakati fulani walipofunga ndoa. Nao—nao waliweka nadhiri zao pamoja. Kisha wakaahidiana, mmoja kwa mwingine, uaminifu wao. Nao wakasema, kwamba, "Tutapendana, kuheshimiana na kuthaminiana, maadamu sisi wawili tungali hai." Lakini ukaja wakati ambapo jambo fulani lilitukia.

64 Mambo haya yote, kuna—kunao wakati jambo fulani linatukia. Na labda nadhiri zao zote, na mashirikisho yote ya mataifa, na kadhalika, labda yalikuwa na malengo mazuri, lakini yote hufikia mwisho wake. Yote yanaporomoka, chini ya mi—mi—miguu ya mwanadamu. Pamoja na malengo yote mazuri tunayoweza kuwa nayo, bali yote hayana budi kufikia mwisho wake.

65 Lakini kuna wakati ambapo mtu anaweza kuja kwenye kitu fulani ambacho ni cha Milele. Hapo ni wakati, mtu, wakati mtu anapokutana na Mungu. Hapo ndipo jambo fulani linapotukia ambalo ni la Milele.

66 Tunafanya makosa yetu. Na tunafanya nadhiri zetu kwenye usiku wa Mwaka Mpya, kuzivunja tu kesho yake. Tunafungua kurasa mpya, na tunaweka nadhiri. Na tunaenda kwa makasisi na . . . Sisi hatuendi, lakini Wakatoliki huenda. Na kufanya maungamo, na kutia sahihi ahadi, kisha tunakuja madhabahuni na kufungua kurasa mpya, bali yote ni bure. Kwa kuwa, wakati mwingine mtu fulani anapotukasirisha ama chochote kile, hasira ile ya kale inaruka mara moja tena. Kila tunapopata shida ama chochote kile, itatokea tena.

67 Lakini kuna mahali ambapo mwanadamu anaweza kufikia, kwenye wakati, utakaombadilisha, Milele. "Yeye atakayekuja Kwangu, sitamtupa nje kamwe," Yesu alisema. Mtu anaweza kumjia Mungu, ndipo kikomo chake chote cha Milele kimebadilika. Naye mtu anaweza kukutana na Mungu,

wala kamwe hawezi kuwa vivyo hivyo tena. Huwezi kukutana na Mungu na ubaki mtu yuyo huyo uliyekuwa. Kama ukimwacha, utakuwa mtu mbaya zaidi kuliko ulivyowahi kuwa. Kama ukimpokea, una Uzima wa Milele, Naye atakufufua katika siku ya mwisho, kwa ahadi Yake.

68 Kulikuwako na wakati ambapo kulikuwa na mtu jina lake Ibrahimu, aliyeshuka kutoka kwa Wakaldayo, na kuishi katika mji wa Uru. Naye alikuwa ni mtu tu, mtu mzuri. Labda, huenda ikawa alininii. . .Baba yake labda aliabudu sanamu, maana walikuwa wametoka Babeli. Naye alikuwa ni mtu wa kawaida tu, naye alikuwa akizeeka. Alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano, naye mkewe sitini na mitano.

69 Naye Ibrahimu, siku moja, wakati alipokuwa labda huko nje kondeni, akiwinda ama chochote alichokuwa akifanya, akichuma maforsadi, ama yoyote iliyokuwa kazi yake, alikutana na Mungu. Na tangu wakati huo, alibadilishwa. Angeweza kuita vitu ambavyo havikuwako, kana kwamba vilikuwako, kwa sababu alikuwa amekutana na Mungu. Alikuwa amejua dakika na saa ambayo alikutana na Mungu. Ilimbadilisha. Ndipo Mungu akamwita kuwa baba wa mataifa mengi. Naye alimwamini Mungu na kuiamini ahadi Yake, kwa sababu alikuwa amekutana na Mungu. Miaka ishirini na mitano baadaye, walikuwa wakijadiliana, wakijaribu kumkasirisha, kumwambia ya kwamba alikuwa ameamini kitu cha uwongo. Lakini Biblia ilisema, "Alipata nguvu zaidi wakati wote, akimpa Mungu sifa." Kwa sababu, yeye alijua ya kwamba ilimbidi Mungu kutimiza ahadi.

70 Hapo ni wakati mtu anapokutana na Mungu. Inabadilisha utu wake. Inampa hisi kuu. Kama nilivyokuwa nikizungumza hivi majuzi usiku, mtu wa kawaida ana hisi tano tu. Lakini, mwaminio, anapokutana na Mungu, yeye hupata kitu tofauti. Ni hisi kuu ambayo humwinua juu ya vivuli. Inamfanya kuamini mambo ambayo hayawezi kutimia. Angali anaamini yatatimia, kwa sababu Mungu alisema hivyo. Mtu anapokutana na Mungu, jambo fulani hutukia.

71 Kulikuwako na wakati ambapo mwanadamu alikuwa amefunzwa katika hekima yote, thiolojia yote ya Neno la Mungu. Aliijua kwa andiko. Alikuwa amefunzwa. Alikuwa na digrii zote. Alikuwa ni mwerevu sana mpaka angeweza kuwafundisha wasomi wa Kimisri pamoja na waalimu wao. Alijua yote, kwa andiko. Lakini mwoga nayo, aliyekuwa akikimbia, akaenda upande wa nyuma ya jangwa na alikuwa akiwachunga kondoo wa mgeni. Lakini ulikuja wakati ambapo Mungu alikutana naye kule, katika kichaka kilichowaka moto. Na kutoka wakati huo na kuendelea, Musa alibadilishwa, kwa sababu alikutana na Mungu katika kichaka kilichowaka moto. Na uso kwa uso na Mungu, asingeweza kuwa vile vile tena.

72 Wakati mwanamume au mwanamke...Sijali ni nadhiri ngapi unazofanya, ama ni kurasa ngapi mpya unazofungua. Mpaka utakapokutana na Mungu, huwezi kubadilishwa. Lakini mara ukikutana na Mungu, basi umebadilishwa milele.

73 Haikumbadilisha tu Musa. Iliwabadilisha Israeli. Iliibadilisha Misri. Iliubadilisha ulimwengu wakati huo, kwa sababu mtu mmoja alikutana na Mungu na kuliamini Neno Lake.

74 Tunachohitaji siku hizi ni mtu kukutana na Mungu, uso kwa uso, na kusema Naye, hali ya mambo. Wanadamu wanapokutana na Mungu, mambo hubadilika. Hakika. Hivyo ndivyo tu tunavyoweza kupata mambo.

75 Na tangu wakati huo na kuendelea, Musa yule mwoga, Musa ambaye alikuwa akitoroka, alikuwa amebadilishwa. Na tangu wakati huo, akawa mtumishi wa Bwana. Daima inafanya kazi jinsi hiyo. Mtu anapokutana na Mungu, mambo yanabadilika.

76 Kulikuwako na msichana mdogo wakati mmoja, si zaidi ya umri wa miaka kumi na minane, au labda si mwenye umri huo, ambaye alikuwa akienda zake kisimani asubuhi moja, kuteka ndoo moja ya maji, huko chini Nazareti. Alikuwa maskini msichana mdogo mzuri. Akaamini. Alikuwa na imani. Lakini, asubuhi hiyo, alikutana na Mungu. Naye Mungu akamwambia jambo fulani, naye akaliamini. Nalo likabadilisha mkondo mzima wa maisha ya huyo mwanamke, na kumfanya asiyepatikana na mauti. Jina lake lilikuwa Mariamu, mama wa Bwana wetu Yesu. Maskini msichana huyo alikuwa ni msichana mdogo wa kawaida tu, bali alikutana na Mungu. Na tangu wakati huo na kuendelea, jambo fulani lilitukia. Bila shaka.

77 Kulikuwako na mtu jina lake Petro, maskini mvuvi asiye na utaratibu, labda mkaidi tu jinsi walivyoweza kuja. Na labda alikuwa ni jitu kubwa mno katili. Kwa sababu, hapa wakati fulani uliopita, niliona ule mchezo, ulioitwa, "Mvuvi Mkubwa wa Samaki." Nilidhani ilikuwa ni maelezo mwafaka sana ya Petro, kwa maana alikuwa ni jamaa mkubwa mno asiye na utaratibu. Hakujali kitu. Ilikuwa ni vigumu kwake kuamini chochote. Lakini, siku moja, alikutana na Mungu. Na tangu wakati huo, alibadilishwa. Tangu wakati huo, akawa mtume wa Bwana Yesu Kristo.

78 Kama vile Ndugu David duPlessis alivyokuwa akitwambia muda mfupi uliopita, kuhusu Sauli wa Tarso, mwuaji, ambaye alilishika koti la wauaji, ambao, na kushuhudia, na kuyashuhudia mauti ya Stefano mfia imani. Alikuwa na barua mifukoni mwake, kushuka kwenda kwa ki—kiongozi wa halmashauri za makanisa, na kuwashika watu waliokuwa wakipiga kelele nyingi kupita kiasi, wakipaza sauti, na kumsifu Mungu. Alikuwa mtu mashuhuri sana machoni pa Mafarisayo. Yeye alikuwa ni Farisayo wa Mafarisayo. Lakini, siku moja,

alikuwa akienda zake Dameski, naye akakutana na Mungu. Nuru ilimwangazia. Na tangu wakati huo na kuendelea, hakuwa tena Sauli wa Tarso. Lakini alikuwa Paulo, mnyenyekevu, mpole, kwa sababu alikutana na Mungu, na ilimbadilisha.

79 Kulikuwako na mwenye ukoma aliyekaa langoni. Tiba zote za madawa zisingeweza kumponya. Vidonda vyake vilivyooza vilikuwa vikubwa sana mpaka mikono yake isingeweza kuinuliwa juu, tena. Nayo miguu yake, ilikuwa ni vigumu kwake kuikokota. Ugonjwa wake ulikuwa hauna matumaini. Lakini alikutana na Mungu, siku moja, akitoka langoni. Naye akasujudia na kuabudu, na kusema, "Ukitaka, Wewe waweza kunitakasa."

80 Naye akasema, "Nataka. Uwe safi." Na tangu wakati huo, hakuwa na ukoma tena, kwa sababu alikutana na Mungu.

81 Kulikuwako na kipofu aliyeketi kando ya barabara. Wala asingeweza kuona mwangaza wa mchana kutoka kwenye giza. Hakuna kitu kingaliweza kumsaidia. Siku moja, mtu Fulani alikuja akitoka kwenye mji wa Yeriko, na alipokutana na Mungu; na tangu wakati huo, angeweza kuona. Macho yake yakafunguka. Uwezo wa kuona mwangaza ulikuwa umeingia machoni mwake, naye angeweza kuona tena. Kwa sababu, tangu wakati huo, wakati alipokutana na Yesu, alikuwa ni mtu tofauti. Aliweza kuona.

Wakati mtu anapokutana na Mungu, kitu fulani hutukia bila shaka.

82 Kulikuwako na kijana mwanamume, wakati mmoja; hapana shaka, raia mzuri wa nchi, lakini mpagao ukamwingia. Naye alikuwa hali mbaya sana mpaka nyumba ya jela isingeweza kumshikilia. Nao wakamfunga kwa minyororo. Naye alikuwa na jeshi la mapepo, ndani yake, hata angeweza kuvunja minyororo na kujiweka huru. Na hao mapepo wakampeleka makaburini, ambako alikaa huko. Naye akachukua vibamba na, akawa mbaya sana, angejikatakata. Loo, alikuwa mtu mbaya sana. Wakati mipagao hiyo ingemwacha, hapana shaka angewazia, "Kwani ninafanya nini hapa?" Na yapata wakati huo, ibilisi angemjia tena, na kumkatakata na kumrarua-rarua. Lakini, siku moja, alikutana ya Yesu. Na tangu wakati huo na kuendelea, yule mwendawazimu wa Gadara alikuwa na akili timamu, amevikwa, akiketi miguuni Pake. Angeweza kurudi nyumbani, kama muungwana. Angeweza kurudi kwenye ustaarabu. Angeweza kurudi kwa wapendwa wake, na angeweza kusema, "Tangu wakati huo, nimebadilishwa." Naam.

83 Ilikukwa ni siku moja, huko Kalvari, wakati Mungu na mauti walipokutana, uso kwa uso, wakati Uzima na mauti vilikuja pamoja. Lakini huo ni wakati Uzima, Kristo, alipoung'oa mwiba kutoka kwa mauti. Na tangu wakati huo, mauti hayajakuwa na mwiba ndani yake. Nina furaha sana kwa jambo hilo. Mungu!

Mungu na mauti walikutana, pamoja. Mauti hayajakuwa vile vile. Hayana mwiba ndani yake sasa. Mkristo mwaminio anaweza kutembea moja kwa moja mbele yake na kusema, "Ee mauti, u wapi mwiba wako? Kaburi, u wapi ushindi wako?" Kwa nini? Wote wawili walikutana na Mungu. Hawajakuwa vile vile tangu wakati huo.

84 Hakuna mtu anayeweza kuwa vile vile, hakuna kitu kinachoweza kuwa vile vile, mara kinapokutana na Mungu. Kamwe hutakuwa vile vile.

85 Ninaweza kukumbuka nikilala hapa kwenye kitanda cha hospitalini. Madaktari walinipa dakika tatu kuishi. Moyo wangu ukipiga, mara kumi na saba katika dakika moja. Nilikutana na Mungu. Tangu wakati huo, sijawa vile vile. Jambo fulani lilinipata. Hakuna mtu angaliweza kuniambia vingine hata kidogo. Bill Branham alikufa. Nilikutana na Mungu, na kitu Fulani kikaingia ndani yangu. Sijapata kuwa vile vile tangu dakika hiyo nilipokutana Naye. Yeye alinibadilisha. Alinifanya kitu tofauti. Haikuwa ni kufanya nadhiri ya Mwaka Mpya, bali nilikutana na Mungu.

86 Wanaume na wanawake, unapokutana na Mungu, unabadilishwa. Tunaweka nadhiri zetu za Mwaka Mpya usiku wa leo; tunarudi kesho asubuhi, kuzivunja; kesho yake, kuzivunja. Lakini tunachopaswa kufanya, si nadhiri ya Mwaka Mpya, lakini tunapaswa kukutana uso kwa uso na Mungu, na kupata Uzima wa Milele, tuzaliwe kwa Roho Wake.

87 Palikuwa na mzee, wakati mmoja, naye asingeweza kujiamulia. Ibilisi aliendelea kumpiga aiondoe kwake. Siku moja, huko nje kondeni, alipiga magoti kuomba. Wakati alipokuwa akiomba, aligongomea kigingi chini. Akasema, "Hiki na kiwe kumbukumbu. Shetani, kama ukija kwangu tena, nitakuelekeza kwenye kigingi hiki. Nami nitakwambia ya kwamba papa hapa nilikutana na Mungu, na lilitatuliwa tangu hapa na kuendelea." Hilo ndilo tunalohitaji, labda si kigingi kondeni, bali mahali fulani, chumba fulani cha siri, mahali fulani. Sio . . .

88 Loo, usiku wa leo, kutakuwako na mamia ya nadhiri zitakazowekwa. Ndipo mwaka ujao itatubidi kuziweka zote, mara nyingine tena. Tutasema, "Tutaachana na kusema uongo. Tutaacha kufanya *hili*. Nasi tutaweka kando hasira yetu. Tutafanya zaidi kwa ajili ya Mungu. Tutafanya *hili*, ama *lile*, ama *linginelo*," tukakuta tu, ni bure.

89 Lakini kile mwanadamu anachopaswa kufanya, usiku wa leo, ni kukutana uso kwa uso na Mungu. Na tangu wakati huo na kuendelea, yeye ni kiumbe kilichobadilishwa. Haleluya! Loo, laiti ningaliweza kulielezea jinsi ninavyoliamini. Lakini wakati mwanadamu anapokutana na Mungu, yeye anabadilishwa, kuanzia dakika hiyo, siku zake zilizosalia. Kamwe hatakuwa vile

vile, kwa sababu yuna Uzima wa Milele. Yeye ni kiumbe kipya. Mambo ya kale yamepita, na mambo yote yamekuwa mapya kwake. Anaonekana mpya.

90 Mgonjwa anaweza kutembea mbele za Mungu, wakati madaktari wamesema, "Atakufa." Lakini anaweza kutembea mbele za Mungu, na kuitetea kesi yake. Naye atatokea, mtu tofauti, na tangu wakati huo na kuendelea.

91 Loo, namkumbuka Mbunge Upshaw, akiketi kwenye kiti cha magurudumu kwa muda wa miaka sitini na sita. Usiku huo, huko California, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka, na kuanza kuzumgumza, yeye alikutana na Mungu. Na tangu wakati huo na kuendelea, angeweza kutembea bila magongo yake.

92 Nimeona wakati ambapo watu walioliwa na kansa walilala, bila kitu ila kivuli. Nao madaktari wangepita pale na kusema, "Wamekwisha." Wapendwa wao wanakusanyika, kusema maneno ya mwisho wawezayo, kwao, himizo. Lakini walikutana na Mungu, na, tangu wakati huo, walibadilika. Wanaishi tofauti.

93 Ninaweza kumwona mwanamke mchafu, huko mtaani. Ninaweza kumwona mlevi, huko vichochoroni. Ninaweza kumwona mnafiki, huko kanisani. Hao watu wote wa aina mbalimbali, kila Mwaka Mpya, wakifungua ukurasa mpya, na kujaribu kufanya kitu tofauti, wakijaribu kufanya mambo upya na kufanya kadhalika. Acha wakutane na Mungu, wakati mmoja, na tangu wakati huo na kuendelea.

94 Yesu aliwahubiria hao tangu wakati huo na kuendelea, walioketi katika maeneo ya uvuli wa mauti.

95 Nami nasema, usiku wa leo, kama mtu anataka badiliko halisi lije juu yake, acha akutane na Mungu uso kwa uso, na kukutana na Yeye wakati mmoja, ndipo anaweza kusema, "Tangu wakati huo na kuendelea, tangu wakati huo na kuendelea, nilikuwa mtu aliyebadilika. Ninajua kwa ujuzi."

96 Katika kitambo kidogo, kanisa litakuwa likikusanyika hapa karibu na madhabahu. Mtakuwa mkiyaweka wakfu maisha yenu, upya. Mtakuwa mkiachana na mambo, na kuweka mambo madhabahuni. Ndugu, hebu nikupe ushauri. Ikiwa hujawahi kukutana na Mungu, uso kwa uso, hebu nikwambie jambo fulani. Wewe kaa kwenye hayo madhabahu. Kaa hapo tu mpaka utakapokutana na Mungu, ndipo unaweza kuelekeza kidole chako kwenye usiku huo wa Mwaka Mpya. Sio, na kusema, "Nilifungua ukurasa mpya. Niliweka nadhiri mpya." Lakini, "Tangu wakati huo na kuendelea, nilikutana na Mungu. Ndipo maisha yakabadilika, na mambo yakawa tofauti. Na kila kitu kikawa kipya, kwangu mimi, tena, tangu wakati huo na kuendelea," wakati ambapo unakutana na Mungu.

97 Sio, kukutana na Mwaka Mpya. Tutakabiliana nao, katika dakika chache, baada ya kitambo kidogo, yapata saa mbili na nusu, nadhani, labda chini ya hapo, tutakabiliana na

Mwaka Mpya, uso kwa uso. Tutakutana nao pamoja na nadhiri. Tutakutana nao pamoja na ahadi. Tutakutana nao pamoja na nia njema. Tutakutana nao, tukisema, "Tutajaribu kufungua ukurasa mpya. Tutajaribu kufanya tofauti." Hayo yote ni mema. Ninathamini hayo.

98 Lakini ndugu, kamwe haitakuwa ya Milele mpaka utakapokutana na Mungu, kwanza. Unapokutana na Mungu, kwanza, ndipo, tangu wakati huo na kuendelea, kila kitu kitakuwa ni tofauti.

Na tuombe tunapoviinamisha vichwa vyetu.

99 Bwana Yesu, Mwana wa Mungu, ninakumbuka wakati nilipokutana na Wewe, Bwana. Ninakumbuka, mtu mnyonge mwenye mashaka, nikiishi maisha mazuri ya uadilifu, sio kukimbia huku na huku, nikinywa pombe, au kucheza kamari, ama kuvuta sigara, ama kadhalika. Lakini nilijua, Bwana, wakati mauti yalipokuja yakinyemelea kwenye chumba hicho cha hospitali, miaka ishirini iliyopita, kulikuwa na kitu kilichokosekana maishani mwangu. Hapo nilikutana na Mungu, na tangu wakati huo. Tangu wakati huo, Bwana, nimejaribu kukutumikia. Maisha yangu yamebadilika na kila kitu kinaonekana tofauti. Nina furaha sana kwamba nilikutana na Wewe, Bwana. Na usiku wa leo, nikiukabili Mwaka Mpya, nina furaha kusema ya kwamba ninaweza kuukabili pamoja na Roho wa Mungu aliye hai moyoni mwangu.

100 Tupe ujuzi, Bwana. Tupe wema Wako na rehema. Tusamehe dhambi zetu. Na jalia tuishi kupitia mwaka huu ujao, Ee Bwana Mungu, tukiwa na ujuzi, kwamba tumekutana na Wewe na maisha yetu yamebadilika. Tujalie, Bwana. Tusamehe kupungukiwa kwetu. Weka ndani yetu Roho Wako Mtakatifu. Tuongoze na utuelekeze.

101 Baba Mungu, huu hapa mwaka wa 1960, unanikabili. Na kuna nafasi kwa ajili ya mkutano wa ulimwengu mzima, ambako kunaonekana kana kwamba makumi elfu mara maelfu, na maelfu na maelfu ya makafiri watupu, ya wapagani, na kadhalika, huenda wakaja Kwako. Ee Bwana Mungu, huku nikiwa na Roho Wako moyoni mwangu, ninayakabili madhabahu Yako, usiku wa leo, na kukuangalia Wewe, na kusema, "Nisaidie, Ee Mungu. Moyo wangu unawaka kwa juhudi. Ninakupenda, Bwana. Ninajitolea Kwako, katika huduma. Niongoze popote unapotaka kuniongoza. Nitume mahali popote unapotaka kunituma, Bwana. Nena tu, nami nitaenda."

102 Libariki kanisa langu. Mbariki Ndugu Neville. Wabariki watu wote hapa, wageni malangoni petu. Na hawa wachungaji watakaokuwa wakinena, wakati baada ya wakati, hata jioni yote, ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utabariki huduma yao. Mbariki Ndugu Neville. Mbariki Ndugu Junie Jackson.

Ndugu Beeler, wahudumu hawa wengine wote, wabariki, Baba. Tupe mwaka mkuu katika 1960.

103 Sisi, Bwana, tunaojua ya kwamba tumekutana na Wewe, uso kwa uso, na tunajua kinachomaanisha kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Wako, tupe neema Yako ya Milele, kukutumikia Wewe. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

104 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mwaka wa 1960, usiuache uwe, ati, "Nilifungua ukurasa mpya." Usiuache uwe, ati, "Najaribu kuanza maisha mapya." Lakini acha uwe, kwamba, "Nilikutana na Mungu, na tangu wakati huo, wakati huo na kuendelea, nilikuwa na amani ipitayo ufahamu. Nilikuwa na furaha isiyosemeka, na iliyojaa utukufu. Nilikuwa na utoshelevu. Hata kama mauti yakinijia, nitakuwa mkononi mwa Mungu, mara baada ya pumzi yangu ya mwisho kuondolewa. Haidhuru kijacho ama kiendacho!"

105 Acha wailipue, Jumapili usiku, wakitaka. Wakitaka kuilipua, bomu halitakuwa limemaliza kutoa vishindo kabla hatujawa Utukufuni pamoja Naye. Amina. Hakuna kitu kinachoweza kutudhuru. Haleluya!

106 Nina furaha sana nilikutana na Mungu. Nina furaha sana ninaweza kusema, "Tangu wakati huo." Litegemeze mahali hapo! "Nilipokutana na Mungu, jambo fulani lilitukia kwangu. Nilibadilishwa, kuanzia dakika hiyo. Nimebadilika, tangu wakati huo." Nina furaha sana kuwa kwenye barabara hii, usiku wa leo, kama ushuhuda kwa ajili ya Utukufu na Nguvu za Mungu. Maskini kitu fulani hapa nje, ndipo Mungu akashuka pale na kunipa mimi neema Yake, na kuniokoa, na kuniponya, na kunijaza na Roho Wake. Na kuniruhusu kuihubiri Injili Yake, ambayo ndiyo heshima kuu sana iliyopo ulimwenguni. Tangu wakati huo, mpaka wakati huu, sijawa na majuto hata kidogo. Lakini nimekuwa na shukrani, siku hizi zote, na nitakuwa, kote katika Umilele, kwamba nilikutana na Mungu.

Mungu awabariki. Vema, Ndugu Neville.

Na Tangu Wakati Huo SWA59-1231
(And From That Time)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza kwenye Mkesha wa Mwaka Mpya, Alhamisi jioni, tarehe 31 Desemba, 1959, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org